

# JARH WAT-TA'DÎL KATIKA ZAMA ZETU HIZI — SHEIKH AL FAWZAAN

---



1. **Suali:**Baadhi ya ndugu wanamsifu Mwanachuoni kuwa ni “mshika bendera wa Jarh wat-Ta’dîl”, kwahivyo yoyote atakayemjeruhi anakuwa ni Majrûh (ameshajeruhiwa) kwa sababu yeye (yaani; Mwanachuoni huyo) huwa hajeruhi mtu isipokuwa kwa dalîl, sasa jee, ni lazima kufuata amri yake katika hilo (yaani; Jarh yake)?

Jawabu kutoka kwa Sheikh Sâlih al-Fawzân (حفظه الله) (Tarehe: 13th Ijmaa Jumâdal Âkhira 1433H – 4th May, 2012):

Jarh wat-Ta’dîl ni (hutekelezwa) katika Isnâd na ‘ilmul Hadîth. Na watu wake (yaani; wanavyuoni wa Jarh wat-Ta’dîl) wameshakufa. Hapana hata mmoja aliyebakia miongoni mwao! Hapana hata mmoja tunaemjua aliyekuwa ni miongoni mwa, ‘Ulamâ’ wa Jarh wat-Ta’dîl.

**Lakini pengine, huwenda wakapatikana ma’Ulamaa wa Ghîbah (usengenyaji) na Namîmah (ubukuzi); hawa wapo - nao ni wale wenye kuwajeruhi watu na kuwasengenywa watu. JAMBO hili SIO Jarh wat-Ta’dîl!!**

Jarh wat-Ta’dîl ni katika ‘ilmu ya isnâd (silisili ya wapokezi wa hadîth), na jambo hili (ta’luma yenyewe) lina watu wake (yaani; watu waliobobeya na kutaalamika kwenye ukumbi huu), lakini hawa (wanavyuoni wa Jarh wat-Ta’dîl) wameshatangulia, wameshakufa ...

Lakini huwenda ikawa kuna mtu fulani mwenye kuvisoma vitabu vya Jarh wat-Ta’dîl, na akafaidika navyo, Naam!

Ama kuhusu kusema yakwamba yeye ni miongoni mwa ‘ma’Ulamâ’ wa Jarh wat-Ta’dîl’ - haya ni MATAMSHI MAKUBWA sana, na hayafai kunasibishwa na mtu aliyeanza kutwalii au kuvisoma vitabu (vya Jarh wat-Ta’dîl) - Hawa si miongoni mwa ma’Ulamâ wa Jarh wat-Ta’dîl (yaani; wanafunzi wa ki-ilmu na watu wa kawaida wenye kutwalii au kuvisoma vitabu vya Jarh wat-Ta’dîl) - lakini inafaa kusemwa, Muttwala’ (yaani; msomi wa kisawasawa, aliyesoma katika) vitabu vya Jarh wat-Ta’dîl, ni hayo tu (yanayoweza kusemwa).” [MWISHO]

Kumbukumbu: <http://www.qsep.com>

Uganisha na kiungo cha sauti:

[http://www.qsep.com/media/alfawzaan\\_on\\_...\\_ay2012.mp3](http://www.qsep.com/media/alfawzaan_on_..._ay2012.mp3):

Mazungumzo yenyewe (ya Sheikh Fawzâ) kwa kiarabu:

يقول: أحسن الله إليكم: بعض الإخوة يصفون عالمًا من العلماء بأنه حامل راية الجرح والتعديل، فمن جرحه فهو المجروح بحجة أنه لن يجرح إلا بدليل، فيلزم اتباعه في ذلك؟  
الجواب:

.(الجرح والتعديل في الإسناد وفي علم الحديث، وهذا أهله ماتوا، (ما بقي منهم أحد

ما فيه أحد فيما نعلم من علماء الجرح والتعديل

لكن قد يكون من علماء الغيبة والنميمة، هذا موجود ممن يجرح الناس ويغتاب الناس، هذا ما هو  
!بالجرح والتعديل

..الجرح والتعديل من علم الإسناد، وهذا له رجاله وانتهوا، ماتوا.. الله أعلم ما أعلم أحدًا

لكن قد يكون فيمن يقرأ كتب الجرح والتعديل ويستفيد منها، نعم

أما أن يقال هذا من علماء الجرح والتعديل؛ هذه كلمة كبيرة ما تنطبق على من يقتصر على المطالعة  
وعلى قراءة الكتب، هذا ما يكون من علماء الجرح والتعديل؛ لكن يقال: مطلع، فلان مطلع على

كتب الجرح والتعديل فقط. نعم

(بتاريخ: الجمعة 13-6-1433 هـ/4-5-2012م)

2. **SUALI:** Muheshimiwa Sheikh, Allâh akuafikiye. Anasema, “Tumesikiya kutokamana na heshima yako yakwamba mlango wa Jarh wat-Ta’dîl umefungwa katika zama zetu hizi?

Jawabu kutoka kwa Sheikh Sâlih al-Fawzân (حفظه الله) wakati alipokuwa akifundisha darasa la al-Muntaqaa (Tarehe 1/11/1434 - 9/7/2013)

Na nyinyi ndio wale ambao mutakaoifungua mukaipa nguvu sasa? Iko wapi Jarh wat-Ta’dîl? Ni nani mwenye uwezo wa kuijua ta’luma hii? Hawana chochote cha zaidi mbali na kuwasengenywa watu na kuwajeruhi. Fulani na fulani ni kadhaa, fulani na fulani ni kadhaa. Huku ni kusengenywa na hairuhusiwi - hii siyo Jarh wat-Ta’dîl.

Jarh wat-Ta’dîl inatokamana na ‘ilmu ya isnâd - isnâd ya hadîth. Ama kuhusu kukaa na kuanza kusema, mtu huyu ni kadhaa na kadhaa, mtu yule ana mas’ala kadhaa - kusifu na kukosoa - hii siyo Jarh wat-Ta’dîl; Hii ni Jarh peke yake, kwani hakuna ta’dîl. Ni Jarh (kujeruhi), Ghîbah (usengenyaji) na Namîmah (ubukuzi) peke yake.

Ref: <http://www.youtube.com/watch?v=mRt7R5Ij4WI>

Abu Farida, Muhammad Awadh Basawad

THE QUR’AN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

[www.qssea.net]